Tunasema hapa, kuna program mmoja Serikali imeendelwa na tungenesema as part of Affirmative Action, as part of encouraging enrolment, as part of promoting education, hii school feeding program, hii Serikali na World Food Programme, imetusaidia nao, ninasikia wanataka kupunguza. Lakini, kama chakula hakitakua kwa shule, watoto wetu hawawezi kusoma. Kwa sababu hakuna kitu cha kurudi kula nyumbani. Kwa hivyo tungependa hio programme iendelee i cover hata ile Secondary Schools zetu. Na kuongeza na bara, bara, postas, stima, na simu, ningependa kuongeza pia stima na maji. Basis Rights Chapter. Hivi vitu tano, iwe lazima. Kila pahali tu tuna Location Headquarters, tunaweka. Tuna nini, tunaweka. Jukumu la Serikali. Hakuna kitu tunaongea tunapanga tena kwa DDC.

Na wakati kuna njaa, tungependa Serikali ilishe watu wake. Vile tulisema, kama hauna kazi, upatiwe allowance kidogo, kama kuna njaa, wanamwaga relief food, vile iikuwa juzi. Nakinai ngiturkana dae ibore ningarakinotori kechi bon neliwor emaidi bon eyenio ainakin

Basi niingie Siasa sasa kidogo. Saa hii mnafanya Katiba, na kweli nimeona umearibu kupanda ndege, saa hii muko karibu pahali tana kwa siku mmoja. Hata sii tano, karibu kumi. Lakini tano Turkana. Muko hata Nandi na kadhalika. Wananchi hawa watu wanahitaji muuda ili waendelee na hii kazi. Tungependa tufanya kura na Katiba mpya. Nikisaki ngakiro na akatiba anakolo ngorot kisaki efanya ekura a katiba anaeyaunitai Na hii Katiba lazima itengenezwe vizuri. Wanachukua maoni saa hii, wataenda kuweka hio report, lazima kuwe na referendum, kuwe na kila kitu, tuaangalie tena. Sisi tumependekeza kama Wajumbe wenu wa KANU, na ninajua nyinyi mumependa KANU, mulichagua, tunasema kwa sababu hata upizani zamani walikuwa wanasema, ‘No Reform, No Election’. Walikuwa wanasema kila hatufanya Katiba, hakuna nini? Hakuna uchaguzi. Na sisi tunasema afadhali kwa sababu tumekaribia, tuongeze hata miezi miwili ama sita tumalize, tufanye kazi mzuri. Wananchi nyinyi munaona je haya maoni? Sisi tungenependekeza mumalize haraka iwezekanavyo kwa muuda munao. Lakini kama itabidii tuongeze, afadhali wa Kenya tujitetee miezi mitatu tena tupate kazi mzuri, kuliko kufanya kazi ambao sio mzuri. Basi hio imeingia ehh?

Ni sisi juzi, na tumepoteza mawadhi kadhaa. Na Bunge juzi imepitisha ya kwamba tuongeze wajumbe. Na vile pia mimi naona ni lazima tuongeze hata wajumbe wa kwetu. Lakini pia ningependa tuongeze Wards. Kwa sababu Councillor inakikana awe karibu na watu. Kwa hivyo tungependa Wards zaidi. Tuongeze Wards pia especially areas kama hapa. Utakuta distances ni

kubwa, councillor mmoja ama chief mmoja awezi kufikia kila pahali. Lazima tuongezewe ma Wards hata zaidi. Na ningependa mishahara ya councillors hapana iwe hii revenue tunatafuta hapa ya (word not clear) wetu imetuumiza sisi. Tunataka councillors walipwe kama wajumbe. (Clapping) Walipwe na Serikali, hapana allowance. Walipwe mshahara kamili. Kama ni shillingi eluf hamsini, wapatiwe kwa mwezi. Kama ni mia mmoja wapatiwe. Kisaki ngoni nakinai ngiturkana kori tolemarai ngiturkana kwa ngitunga luche dae nyo arakari ngiturkana imuriakinitae

Halafu tunasema hivi, lazima pia tupate sheria ambao kama councillor amechaguliwe na huyo councillor amepotea njia, kama councillor ame defect, kwa yule mjumbe alichaguliwa na yeze ama mjumbe awache chama ambacho kilichagua yeze, awache laini ya rais, huyo councillor anatakikana aachishwe kaji mara moja. Uchaguzi ifanywe tena. Kwa sababu uongozi unahitaji umoja. Kama tulienda kura tukiwa team moja, lazima tufanya kazi tukiwa team moja. Itakuwa mbaya mimi kama mjumbe, nianze kuwa na shuguli ingine tofauti na ile ya rais. Na councillor awe tofauti na ile ya mjumbe. Huyo mjumbe, huyo councillor wanatakikana warudi kwa wananchi tuamuwe mambo yake tena. Ninasema hayo nikiwa sasa nyumbani hapa. Kwa sababu kuna ma councillors, baadala ya kuambia watu ukweli, utakuta mambo kama haya. Tunaongea mambo ya Katiba. Baadala ya wazee kuja kueleza maoni yao ketingiti itwan ikoni koku kape kijau ngibaren kiboyo arai ekichul ibore a ngiturkana mere aka katiba, ngikarikok eunito ngakiro nu. Keyaunit itwan akou yau taramai akitoe eyangakisi

Tungependa mambo ya, unajua sisi Karamojong hapa ni kama Watukana tu. Na kwa sababu ya amani ile tumeleta, tumekua na uhusiano mzuri. Na utakuta Uganda kwa kweli watatushinda sisi kama Kenya. Wame decentralize decision making mpaka kwa Parish, mpaka kwa County, kila kitu, maneno ya resources yao, wanapanga hapo. Sisi pia tungenesema hivi, hayo maneno ya DDC ya DSG, ya Leaders Meeting ni kazi bure. Tunaongea mambo na hatuna budget. Tunasema tuweke bara bara pale, engineer ndio unakuja kutengeneza, ujui amekula ngapi? Ujui anatumia ngapi? Sisi tungependa accountability. Tungependa kama ni leaders sisi wale wamechaguliwa na watu, tuwe na

public servants pamoja. Wakati ya hii inakuja inaletwa kwa meza. Ili tujue agriculture ni pesa ngapi? Kweli sisi wajumbe munatutuma Nairobi, tunakagua, tunasema agriculture patia, pesa fulani. Lakini wakati unakuja Wilaya, hatuna uwezo. Na sisi tunakuja kwa wananchi munatuambia tengeneza bara bara, fanya hii na kuna mtu mwengine anafanya hio kazi. Kwa hivyo tungependa decentralization ya resources, ya budget, kila kitu ikuje kwa District. (Clapping). Ili tugawe pesa pale tukiija District pia tuseme Kalokol Division inapesa kiasi fulani halafu viongozi wa Kalokol wataamua tujenge shule, tujenge hospitali, tujenge bore hole ama nini kulingana na mahitaji yao. (Clapping)

Halafu tungependa pia ile sheria itatoka baada ya hii Katiba. Wale watu wanadanganya sisi, wanalete ile cheque, tunapiga makof, na ina bounce. Hiyo sheria tunataka itengenezwe. Hatutaki kudanganya wananchi. Kama hauna pesa, hauna pesa. Kama una pesa, una pesa. Kama unalete cheques ambae ina bounce, lazima wewe upelekwe mbele. Kwa sababu hio ni kutudanganya.

Tungependa pia, kuwe na sheria ya kwamba kuna wakati wa campaign. Kama kuna wakati wa campaign, tufanye uchaguzi na

baada ya uchaguzi, lazima tukuwe kitu kimonja. Wilaya hii, na nafikiri Kenya nzima, kazi ya upinzani ni kutukana Serikali. Siku ya kwanza mpaka siku ya mwisho. Kazi ya watu wengine hapa ni kutukana wajumbe, ni kutukana councillors, ni kutukana chiefs. Mam ngakiro ianio ngirwa lu atamar mam ngache aloturkan atamar be atona akop, ngai aari tamayo iyong emjumbet. Emjumbet kolong earene akop, mam kolong ache atamar emam akiru. Esiasa kidich ngoni kutoka 98 tani 2003

Tungependa sheria iwe sheria kabisa na wale watu wanasumbuwa watu lazima tuangiliwe mambo yao.

Mambo ya Harambee: Sisi tumesema hii na siasa pia inatufuata. Sisi tulikataa Harambee hapa. Na hatukukataa harambee ya kujenga shule, ya kujenga hospitali, kile kitu inaonekana inasaidia wananchi. Tulisema tutafanya harambee kama hio ikisaidia miradi ya watu na mzazi ataleta hata kama ni mbuzi, kama ni mkeka, kama ni samaki, alete, tunapiga mnaada. Ile harambee tulikataa ni ile ya kutumia nguvu. Ile ya kutuma askari kwa wazee kutafuta mbuzi yao. (Clapping)

Na ningependa kurudia hayo. Kwa sababu zamani harambee hapa ilikuwa DO anaenda transfer, tunataka harambee. Na hio ni kazi ya Serikali. Kama Do anaenda transfer, Serikali itume pesa, tunaweka party yake wapeleke mtu wake pahali wanataka. Ibaki harambee ya shule, ya hospitali, ile unajua mtoto wako anaenda, ufanye hio harambee. Kwa hivyo ngikasukou itwan ni ebala iyong be engerit Ekwee harambee nangeriti ayong harambee nakolong a ngatochio na ilatai nakware eangasi ngikatukok ngirwa lu

Ningependekeza pia ma Chiefs lazima Chiefs pia wapitie ile bara bara sisi napitia kama viongozi. Miaka mitano, waende kura. (Clapping) Kwa sababu siku hizi utakuta Chief ameringa na hii Crown kabisa. Anasimamia hata yeye, Minister wa Serikali, ati mimi ncio macho ya rais. Na hata rais hajawaandikia hawa baruwa. Na mimi ndio rais amenipatia baruwa ya appointment. Na anatakikana kuhudumia watu. Anaandika karatasi huko, pengine ni rafiki yangu, mimi napoleka jina huko, analetwa. Sasa hana heshima na wazee. Tunataka baada ya miaka mitano turudi, kama ni mzuri tatarudisha. Kama amekosa apate brake. Eee! Kori ai? Tarama eripot ni a Dc egela akop

Baado bwana.

Com. Lenaola: I have a long list.

Hon. David Ethuro: Kuna Mayo: Tunataka Councillors wachaguliwe. Wale wa municipality tuwachague baada ya uchaguzi huo. Tunataka haza ma Mayors, kwa sababu hata sisi tunaishi Nairobi. Ningependa pia nafasi nichaguwe Mayor wa Nairobi. Nichagwe pia Mayor wa wapi? Wa Lodwar. Sisi wananchi. Kutoka wale Councillors tumechagua. Hapana Councillors ndio wanachugwa Mayor. Hii imeleta taabu yote. Kwa sababu leo, wanasema ni Ejore, kesho kutwa wanasema ni Reverend. Siku hio ingine watasema mtu mwengine. Mpaka hakuna kazi inafanyika siku hizi. Kazi ma Councillors wanafanya ni kupigana tu kuwa Mayor. Lakini kama ingeletwa kwa wananchi, nafikiri hio itakwisha. (Clapping)

Tungependa pia mwenye kiti, hivyo, hivyo pia kwa Mwenya Kiti wa County Council. Councillors wachaguliwe kutoka kwa hawa, tuamuwe wale watakuwa Chairmen. Tupige tena kura sisi zote, tuchaguwe nani? Mwenye Kiti.

Na kwa sababu siku hizi inaonekana wananchi hawana imani na hii Location Development Committees, ama Sub-DDC'S. Siku hizi ni kwa Mheshimiwa. Mheshimiwa dawa ya hospitali, Mheshimiwa nini, akitoka kwa Mheshimiwa anaenda kwa Councillor. Akitoka kwa Councillor anaenda kwa Chief. Sisi tungependekeza hivi katika Katiba mpya, lazima kila Constituency ipatiwe fund ya development yake. (Clapping) Ili mimi nikiwa Mjumbe hapa, niweze kuwa na Kamati yangu, tuseme katika Constituency yetu tumepatiwa na Serikali pesa kiasi fulani. Basi tuketi tuamuwe kama ni ku rehabilitate the Society, tuweke pesa hapo. Kama nikufanya kitu fulani, tufanye hio. Nafikiri hio itatusaidia. (Clapping: Kwa sababu hizi pesa zinapotea Nairobi. Na sisi hatupati hizo pesa.

Ningependa tu kusema wakati wa uchaguzi, lazima tuwwe na polling stations. Watu wetu wanatembea. Pengine wapepiga kura leo, Kalokol mahali walikata. Hio Kura itawapata Lokichogio kulingana na hali ya anga. Ingekua vyema, wakati wa Kura, kuwe na polling stations, kama zamani. Ile uchaguzi ya 1974. Tulikuwa na mobile polling stations. Watu wapige kura bora unaona kila kitu iko sawa, sawa, hio marks iwe ile asipibe mara mbili tena. Hio ionekane na watu wapige, hio itafanya watu wengi wapige kura. Kwa sababu hii ni muhimu kwetu, sisi Bunge tunachukuwana ka Wajumbe wa watu kutoka hapa. Watu wanasema watu ni wachache. Lakini kwa sababu Kura inakuja wakati watu wetu pengine hata wameenda Uganda kutafuta nyasi huko. Sasa kama mobile polling stations ilikwako ingetuaidia.

Mimi naona siku hizi, mimi sielewi kazi ya Chief na ya DO siku hizi. Si elewi kabisa. Na kazi ya Police. (Clapping)

Kwa sababu badala ya kuchunga amani, kazi ya police ni kwenda kwa busaa kusumbwa akina mama. Kazi ya police ni kusimamisha ma gari kwa bara bara na kuchukwa rushwa. (Clapping) Kazi ya police, wewe unapigwa unaenda kupiga report, wanachukuwa pesa kwako. Yule alipigwa wanachukuwa pesa kwake, yule alipiga wanachukuwa pesa kwake. (Clapping) Sasa hakuna mtu anaokoa mwengine. Mimi Ningependekeza namna hii. Lazima tunafanya overhaul ya Adminsitration na hio ya police, tupate unit mpya kama Uganda vile wamefanya.

Nikimalizia ningependa kuja kwa maneno ya two term limit ya President. Mimi, hayo ni maoni yangu binafsi na mtaniunga mkono ama mukatae, lakini mimi ningesema hivi. Kweli hii nchi tunataka iwe democratic na tunaendelea. Tunafanya reforms ya Bunge. Tunafanya reforms ya Public Service. Tuneleta ile Bills ya Ethics, tungependa. Lakini kuna wale wazee wetu walitufanya kazi mzuri ya kuleta uhuru, na Kenyatta akiwa rais, alishikilia hii kazi mpaka akalala. Mimi naunga two term limit kwa President lakini kwa ile generation yetu, ile ya dot.com, ile ya young turks. Lakini kwa ile ya generation ya zamani, ile ya President Moi, sisi wengine tungependelea aendele mpaka alala kwa kiti halafu baada ya hio, sisi tukule ile mbili halafu tunaenda kupumzika. Asante sana.

Com. Lenaola: Asante Mheshimiwa kwa maoni yako. Jambo la kwanza, tungependa kusikia maoni yako kuhusu mvumo wa Serikali. Ningependa Serikali ya aina gani katika nchi mpya ya Kenya? Jambo la pili, hukueleza vizuri ungependa nini kuhusu ma DO na ma Chiefs? Umesema kwamba kwa police kuwe na system mpya ili wawe wanaangalia watu vilivyo. Lakini haukusema vizuri kuhusu ma Chiefs na ma DO'S. Tungefanya nini? Tujaribu ku overhaul pia wao na kama ni overhaul, overhaul ya aina gani. Nafikiri itatusaidia sana.

Hon. David Ethuro: Asante Bw. Commissioner. Kuhusu DO na Chiefs, mimi nilisema ma Chiefs mimi naona wanasaidia kazi ya maendeleo kweli. Hatuweze kusema wote ni wabaya. Ile tunasema tu ni kwa sababu wameandikwa, wameandikwa na mtu mwingine, ndio inaleta taabu. Tunasema tu wapigwe Kura kama Councillor na Mjumbe ili wa renew hiyo mandate baada ya miaka mitano, waendelee. Yule afanyi kazi na wananchi, wananchi wanaweza kuwa na nafasi ya kumwambia apumzike. Lakini yule anafanya kazi, aendelee. So hayo ni ya Chiefs. Na kwa sababu Chiefs, ni watu wetu wanatoka kwetu, na ni vile yule mama alisema pia, lazima kuwe na vetting. Lazima tuwe na system ya kwamba wazee wa hio Location wanaweza kukaa na kupendekeza kama majina matatu and then hayo majina matatu ile imetoka kwa wazee ya hio Location, ndio wataenda mbele wafanyiwe interview kulingana na ile recommendation ya watu ya hio Location. Hiyo itaonyesha ya kwamba watu wenyewe waliamuwa hawa. (*In Kiturkana*)

Nafikiri itasaidia.

Kwa DO, kwa DO kwanza sisi hapa Kalokol, sisi hatuwahi kupata DO mzuri. DO wakati wa maendeleo anatutoraka. Wakati tunasema hii Society tutengeneze, samaki yetu iwe hapa, DO anatakikana atusaidie hio, hawatusaidii. (*in Kiturkana*)

Kwa hiyvo munaone hio system ya ma DO na PC ifutuliwe mbali. Sisi from here stright to line Ministry.

Mvumo wa Serikali: Nilikua nimesahao hio kweli. Sisi tunataka a Parliamentary System. Tunataka mamlaka mengi ya saa hii, na hii ndio sababu tunataka hii Katiba ibadilishwe, na tufanye Kura kulingana na Katiba mpya. Kwa sababu saa hii, hata Pope akipatiwa madaraka ya ile President anapatiwa saa hii atawowa wanawake kumi. Baadala ya kuwa bila. (Clapping).

Tungependa hio madaraka igawanywe tuwe na President, tuwe na makamu wake na tuwe na Prime Minister ambae Prime Minister atakua Head of Government, ye ye ndio atakuwa mkubwa wa Serikali. Na Prime Minsiter awe mtu ambae tunachagua kulingana na MPS wa chama fulani. Kama Wajumbe wa KANU wako wengi, basi, hicho chama kiunde Serikali na mtu ambae, mkubwa wa Serikali awe Prime Minister halafu President atakuwa tu overall. Sasa ye ye ndio atakuwa mkubwa Parliament, mkubwa wa Majeshi, na mkubwa wa ile, ile kazi ingine. So Hiyo ndio system, mimi ningependelea itatusaidia. Itatoa mamlaka, itagawana kulingana na, wapi hii Mr. Alfred, Mr. Alfred aliongea kabisa. Ee! System kama hiyo. Nafikiri itatusaidia. (Clapping)

Com. Lenaona: Kwa moyo huo, huo wa uvumo wa Serikali, structure ya Government, kwa sababu umesema kwamba ma PC watolewe, ma DO watolewe, ungetaka Serikali iwe namna gani? Sio, uongee develution of power. Utuambie devolution ikuje upande gani? Ikuje kwa Local Authority, ije kwa Province, kwa Majimbo, ibaki Serikali kuu, ama aina gani?

Hon. David Ethuro: Mimi, sioni faida ya Majimbo in terms of Federal Government. Lakini mimi naona kuna umuhimu ya devolution ya power. Kama tutafanya kama County Councils, iwe Local Authorities hio, na tupatiwe nguvu, District ni kitu ya muhimu kuliko Province. Mimi sioni kwa kweli faida ya Province. Utakuta DEO hapa, District Education Officer, anapitisha mambo kwa Provincial Education Officer, huyo kazi yake tu ni kuitisha barua iende Nairobi, faida gani? Tunataka kutoa toa hii takataka iko katiki hapa. (Clapping) Ili communication kutoka kwa Central Government, straight wapi? Kwa District. Ee! Provincial layer ni administrative cost tu, pesa mingi na haina maana. Hakuna kitu inasaidia. Natunalia hakuna pesa kama Serikali. Si lazima tuangalie tutatoa nini na nini ili tubaki na kitu kidogo. Tupatitie watu vitabu, karol, Ee!

Com. Lenaola: Asante sana Mheshimiwa nadhani ---- asante kwa maoni yako. Haya tumsikie sasa Samuel Ebei. Samuel Ebei.

Samuel Ebei: Ni Samuel Ebei. Nimachache tu nataka kusema juu ya mambo ya watu ambae ni walemvu. Ni muuda sana hata tangu baada ya uhuru, hata kabla ya uhuru, hapa Turkana hatujawai kuwa na mradi yoyote ya maendeleo ambae inasaidia kwa njia ya walemvu. Hasa kama vipofu, vilema hata shule ama hospitali, ama Nursery yoyote yakuwawekwa walemvu kwa sababu mpaka saa hii kuna wengine wanaishi mbali sana na hapa urban area. Hapa Kalokol ni town. Kuna watu wanakaa sehemu kama Kakua ama na Kulei na kuna walemvu na vipofu. Serikali aiwezi kuwa inahitajika ipate nafasi ya kuwasikia ili hawa watu waweze kusaidiwa angalau, wengi wao kwanza ni watu hawajiwezi.

Pia, ningependa kusema mambo mengine kuhusu mambo ya police. Unapata kwamba police wametupulia mbali sheria ambao inahitajika ama orders ambao wamepewa na Serikali watumie. Inafikaga kiasi kwamba unaenda na ukifika katika station ya polisi, unapata kwamba police akiwa individual pekee yake akiwa fulani, either fulani ama anaitwa Kamau, hio sheria sio sasa ya Kenya, inakuwa ni ya Kamau, ana handle vitu vile anavyo taka kwa sababu hata kwanza ukiwa umekuja umeleta complaints fulani, unapata kwamba hio complaint aitiwi maanani. Unaone kwamba kitu cha kwanza ni kuangalia upande wa rushwa. Rushwa huku kando, kando na hali kadhalika wewe ambae una stahili kusaidia, hausaidiki kwa njia yoyote.

Pia, kuongezea, ningeongezea juu ya misaada ya NGO'S hapa hivi kama sasa relief ambae inafikia Watukana upande huu. Sisi tungependelea chakula ya relief wakati inakuja. Hii chakula iwe free kwa kila mtu at least tuone ya kwamba hii chakula inapewa authority ya wazee, wazee wetu wa mtaa ndio wawe wanasmamia kwani, ndio wanaoelewa kwamba ni nani na nani ambae amelemewe zaidi. Kwa sababu mzee wa mtaa yuko karibu na sisi. Anajua ni nani anakuliwa na njaa au ni nani hajakuliwa na njaa kwa sababu yuko karibu na watu. Unapata kwamba kuna wengine, ambao kwamba anajiweza, mtu ana duka ana maduka na unapata kwamba yeze ndio an reliefiwa zaidi ya mama mmoja ambae hata hana mtoto wala ajiwezi.

Pia, ningependa Serikali yetu, itie maanani saana juu ya mambo ya uajiri wa kazi. Vijana wengi hapa Turkana, wamesoma na hali kadhalika mpaka sasa, kuna upungufu wa kazi, kuna upungufu wa kazi kulingana na nini? Kulingana na miradi za maendeleo ambao aipatikani hapa Turkana. Kwa hivyo Serikali inatakiwa itumpe miradi mbali, mbali za maendeleo ili tupate nafasi ya kuajiriwa kazi. Asante.

Com. Lenaola: Asante sana. Mark Kioko. Mark Kioko.

Mark Kioko: Asante sana. Kwa vile wengi wameongea. Kwa majina kwanza naitua Mark Kihos. Ningependlea ---- mahali pengine ambako ametajua halafu na maoni ---

Kitu cha kwanza ambacho ningeweza kusema ni President must be above the law for the following :-

He as the only man has the power. He can control and anybody opposed the required level of living standards e.g. opposition leaders whose aim is to jeopadize this Country.

This is a chance to minimize the mushrooming of fake and bogus opposition role leaders qualities.

Anything wrong to the President must be left out until his time of re-election period.

Jawabu ya pili: Chief must be elected by wananchi themselves.

Village Elders must prevail so as to make them please and encourage the smooth running of the ----- at the grassroot's level.

Dowry expenditure must be left the way it was (words not clear)

Education in Turkana and other arid areas to be left free to increase the numbers --- in Kenya.

Chief: Leaders through Electoral Commision of Kenya must be leaned for easy running of our Country.

Kabla ya number saba. Period of Constitutional amendment to be increased for enough time to fulfil his work.

Ya nane: The President atufikirie sisi Waturkana kwa kutuchagulia waziri from the ruling party badala ya Assistant Minister kila siku ama kila wakati.

Assistant Chiefs and Councillors must have their offices to minimize domestic problems taking place.

Ya mwisho ambae ni: We have Lake Turkana in Turkana District hence Choro Island should be left for Turkana District than Marsabit District. Asante.

Com. Lenaola: Hamna maswali. Asante sana Mark nenda ujiandikishe. Marikon Amadi. Marikon Amadi.

Marikon Amadi: ejok robo esi daang, ekang kiro Mariko Namadi. Eya ngirotinit lukibwalar ngoni ngiraya a lowahi alokalapatani kalo lu itemokino atolimokisi nangolenyang natokona a katiba ana kitetet kana kingolik. Ngirotin ngullu ngesi tokona lu

Translator: Sisi tukiwa Waturkana kwa kweli tumekuwa marginalized na tukiwa raia kuna njia tofauti, tofauti ambazo tumenyanyaswa na Serikali na njia hizi, njia ya kwanza ni,

Marikon Amadi: lo ekingareni ngesi lo egeri eche na earia itwan ni a ngaropiae anierumor kisieunia ngaropiae nakot anielosi itwan ni arai ngesi earitae itwan keng ani elosi ama kipararakinae kotere mam ngaropiae eya toliwor nabo itwan ni ngarakinio ngesi ni earit itwan

Translator: Sheria lazima ikuwe inafanya kazi kwa kila mtu. Kwa mfano kuna wakati fulani mtu anauwa mtu. Sasa mtu yule muuwaji, anakimbia anapeleka pesa ama rushwa kwa Koti. Na yule ambae amewawa watu wake wakija ku complain, kwa sababu hawaja peana pesa zozote, case hio inatupuliwa mbali, kwa sababu huyo mtu hajapeana pesa. Kwa hivyo tunataka sheria iwe iwe ina govern kila mtu.

Marikon Amadi: na ngarei egeri eche eyei nabo akampuni ache na ebumene abwelar nabo ngitunga nabo lu a ngakiyosikio ngulu lu arai akisiekin ebishara kech ngina be ne ponere akingolikini iche bore be ngaratilia anielosio tamarai erono aratil ngina. Kisaki nangolenyang tachaka ngakiro nguna

Translator: Katika Serikali yetu kuna Wizara ambae inashugulika na mambo ya kupima mitaani. Kuna authority fulani ambae inahusika na mambo kupima mitaani. Yeye angependekeza kuwa Wizara kama hio itupuliwe mbali hakuna haja kwa sababu inanyanyasha wananchi katika, wale wako chini, inapenda kunyanyasha wananchi saana.

Marikon Amadi: ngakiro na ngauni ngakiro a kot ani eyei tokona ngirwa lu kisaki tokona engolenakis kingoliki ngakiro a kot . kisaki nangolenyang tosubaki ngakiro nguna nelemun mono ngaropiae

Translator: Tunataka pia mambo ya Koti, kuamuliwa kwa case, isiwe kwamba pesa kwamba zinatolewa kabla ya case aija amuliwea. Pesa, ama fine itolewe baada ya case kuamuliwa.

Marikon Amadi: nakang dang ngesi nguna arai takae ngauni alimunit. Kingarakinite Akuj

Translator: Maoni yangu ni hayo.

Com. Lenaola: Asante sana Bw. Amadi. Nenda pale ukajiandikishe. Gabriel Ekai. Gabriel Ekai.

Gabriel Ekai: eani ayong a ngakiswahili ka ngaturkana. Wazee na mama Hamjambo.

Com. Yano: Hatujambo.

Gabriel Ekai: Asante sana kwa kufika kwa Katiba ya leo na tumeshukuru kutufikia kwa Katiba ya leo. Nitaenda machache katika hayo. Nafikiri ni hivi ama tano. Tumeshukuru kwa kujenga shule kwa kufanya harambee ambao tulijenga shule. Na hio harambee tulifurahi sisi wote mpaka hata wale ambao walienda ng'ambo tulikuta kama wanaimba tu tukisema tulifanya harambee ya maana saana. Karibu ni million tu. Tuseme ni millioni tulifanya.

Lakini, lakini, tuko sasa uangamishi wa upande wa kuvua kwa hii mlima hii. Sisi zote ni kama wavijana. Tunaenda huko tunanyanganywa nets na wale ambao wananyanganya sisi nets ni Serikali sio hati si Serikali. Unanyanganywa net na unarudi tu unakaa hapa tu na unaji hangaa hanga tu. Una shindwa hata na kukata kuni. Forest imefika, unajaribu hata kwenda kuiba, unashikwa unapelekwa kwa police. Sasa utaenda wapi? Utangamia Kariba gani sasa ambae inaweza kutusaidia? Na mnaleta Katiba.

Tunataka mutusaidie hivi. Kama ile ni Serikali ambae inatusaidia sisi wote wananchi atuwachie nafasi ya kuvua kila mahali, kila upande tufike. Hata kama ni Ethiopia tufike. Hata kama ni Uganda tufike. Mboona ukienda Uganda, ukienda Uganda, kama juzi tulipeleka samaki Uganda, Busia, unatembea tu, unatembea tu mpaka Uganda kwa border unatembezza, unarudi. Hakuna matatizo yoyote, unatoka salama. Na mboona hapa ndani ya tumbo, unasikia tumbo pande mmoja inakuumma. Na hio tumbo yote, inatoka kwenye sheria ya Serikali yetu?

Haya ya pili: Serikali itusaidia kila upande wa pembe. Itusaidie. Itufungulie. Itufungulie biashara yetu. Ukienda ukipata shillingi elufu mbili, uanze na hizo shillingi elufu mbili yako, kununua nguo, kununua viatu na kutembesha na kusaidia kwa kila njia.

Ya tatu: Serikali itusaidie upande wa shule. Shule iwe bure bila malipo yoyote hata ndururu, kuanzia Nursery mpaka Std. 8. (Clapping).

Ya nne: Tunataka Serikali ikiwa District Hospital ama ikiwa Dispensary, yote iwe haina malipo yoyote hata moja. Iwe free. Tukunywe dawa. Ukigonjeka ukifika tu kwa hospitali, hata kidonda, kidonda pekee yake ambae miba imekuchoka na imefura kidogo imetoa utaa. Unambiwa lete shillings mia mbili hamsini. Mia mbili hamsini na nimekwambia hii ni kidonda bwana. Unaweza mwaga hata spirit pekee yake. Na unambiwa lete mia mbili hamsini.

Haya ya tano: Serikali itusaidie kwa hio njia yoyote. Asanteni sana.

Com. Lenaola: (in audible) Chief Longole yuko wapi?

Mr. Long'ole: Mimi naitua Long'ole. Jambo la kwanza

Com. Lenaola: Because you have a memorandum, just highlight.

Mr. Longo'le: First of all our former Constitution starts with ‘Kenya is a sovereign State’ na sasa hii Katiba mpya mimi ningependa kusema hivi. It should start with ‘We the people of Kenya’ ‘Sisi watu wa Kenya’ Isianze kwa kusema Kenya is a sovereign State’ kama vile hata America wanasema kwa Constitituion yao kitu inaitua Preamble. Wanasema, ‘We the people of the United States’ therefore ‘We the people of Kenya’ we want so and so.

Secondly, we want a Pastoral Ministry to be initiated for the Pastoralists. Hiyo walikuwa wamesema.

Two, we want terminal benefits kama pension, mtu aki achishwa kazi ziweze kuleta kwa District, sio tu unaenda Nairobi, those terminal benefits we want them to be decentralized here.

Things like I.D. Cards, Passports, Driving Licence and other key documents, we want them to be issued in the District Headquarters.

Again, issues to do with Public Service, we want the Public Service Commission to decentralize each activity in the District.

Again, coming to the issue of Defence and National Security: Tunataka Serikali waweze kupeleka Army, Military and Para-Military to the International Borders sio police.

Again, we want in this Constitution to be initiated District Internal Security Committees. Zamani kulikuwako na Security Committees. Wawo watasaidia wanajeshi kulinda borders zetu ama *ewa lo a ngimarile yege ewa lo a ngitoposa ama* So the Security Committees should help the para-military committees to guard the International borders.

Secondly, we want compensation to be initiated by either Government either the Foreign Government or the Kenyan Government in case the relatives and the properties of people were destroyed in the cause of the fights.

Again the compensation the compensation fund to be initiated, to be created, to be entrenched in the Constitution iwekwe kwa Katiba. It is not there.

Lastly, Ombudsman's office. This office should be created in the Constitution. This will enable mtu akiwa na shida anaweza kwenda kwa huyu mtu na huyu mtu awezi kumtetea. Ningependa hiyo ofisi iwekwe kwa Katiba. Halafu hio ofisi tena iwekwe kwa kila Wilaya. That office of the Ombudsman should be decentralized in every District.

I want the Kenyan Government through this Constitution to initiate what we call socio-economical programmes for youths. Vijana saa hii hawana muelekeo Sisi kama vijana hakuna muelekeo. We want the Government to initiate hizo socio-economical programmes for us.

Again tungependa, the right, in this Constitution we want to have the right of the orphans. Tunataka watoto mayatima ngide lukokiok.. The fund should be created for them. The Government of Kenya should create funds for these people. Naki ngide lu ngaraopiae

Halafu, coming to natural resources. The boundaries demarcated. The boudaries demarcating Lake Turkana should be redrawn because Islands like Marsabe, Central Island, Southern Island, and Northern Island, zote ziko kwa upande wa Marsabit District na sisi hii bahari yetu wametaja kwa jina letu. Therefore we want these islands to be for the Turkana and the Lake also to be for the Turkana. The proceeds from these Islands and other tourist attraction should benefit directly the Turkana community. (Clapping)

Com. Lenaola: Last two points.

Mr. Longo'le: Mambo kuhusu ma Chiefs. Jambo la kwanza ningependa Chief awe elected na watu.

Jambo pili, Chief awe amefanya kazi kwa miaka kumi.

Jambo la tatu, Chief awe ni mwenyeji wa hapa.

Jambo la nne, Chief awe amesoma. Awe Form IV. Asiwe tu raia. Chief should be subejcted to language test. Afanye mtihani. *Mere abunere akiyan echafu alotunga aluisomato* Halafu, the Chief should be thirty-five years and above. Lazima awe na

miaka thelathini na tana kwenda juu ndio mtu aajiriwe awe Chief.

Ya nne, Chief akifanya what we call the breach of the Constitution, he should be removed from office by pass of vote of no confidence. Atolewe kwa ofisi na watu.

Com. Lenaola: Last point.

Mr. Longo'le: Halafu, ya mwisho, nakuja kwa Councillors. Councillors wawe elected. Na Councillor lazima awe amefanya kazi kwa miaka kumi. Councillor ni lazima awe amesoma. Awe ni mtu wa Form IV. Awe ameenda College ama whatever. Therefore Councillor also should be subjected to language test. Afanye interview. Akianguka, shari yake.

Halafu, ya mwisho, na Councillor saa yoyote atolewe kwa ofisi iwapo kama hatataekeleza yale wananchi wanataka. Watolewe na pass of vote of no confidence.

Ya mwisho, ningependa kusema the issue of nominations. Nominated Councillors, nominated MPS, itolewe kwa katiba ya Kenya. Hatutaki kusikia hio. Hawa watu wawe elected. Wafanye kura yao na watu wachaguliwe na watu. Sio, kuchaguliwa na Rais ama nani. We don't want that. Thank you.

Com. Lenaola: Go there and sign. Nataka kuwajulisha kuna watu ambao wamefika hapa. Simama. Leah Abenyo.

Leah Abenyo: ekiro kang enyaritae Leah Abenyo

Translator: Kwa majina anaitua Leah Abenyo.

Leah Abenyo: *emam nasaki ayong alimuni, alimuni ngauni*

Translator: Ana maoni matatu hivi.

Leah Abenyo: asaki alimuni kona atamar kane alo turkan eponenete ngakampunio neke turkan kiwokunai ngitunga ani kalononi na kechi ewikinito ngitunga na neke turkan mam ngitunga lu isomato lu edodorete aweikini ngitunga ?

Translator: Pendekezo lake la kwanza nikuwa hapa Turkana huwa na ma company mengi ama ma NGO'S mengi ambao wame ingia hapa. Na unapata kuwa watu kutoka mbali, kutoka sehemu zingine za Kenya wanapata first priority ya pengine ya kuajiriwa kazi au kutekeleza mambo mengine ya muhimu. Je mboona sisi tusipewe nafasi hio? Ya kufanya kazi au kupewa nafasi ya kazi. Tuwe beneficiaries ya kwanza. To benefit kwa hizo projects ambao zimingia.

Leah Abenyo: tokona arai alemunit napas kama alo lokichogio itembeete koche kongina emam ekas lakini kisomato kechi togela ngitunga lu eweikinito nafasi a ngikasia ka ina ekaasi kech akiyok ngikch kori akiyok akiwanja

Translator: Ka mfano katika Wilaya hii ya Turkana, kuna sehemu inaitwa Lokichogio, kuna ma company mengi, ambao imeingia huko. Unapata watu wengine ambao wametoka sehemu zingine za Kenya ndio wanachukua nafasi, wao wanapewa tu kama ni auxilliary staff ama subordinate staff ya company fulani, wanafanya kazi ndogo, ndogo na hawa watu wameshoma na unaona wamefika kiwango cha wale ambao pia wanafanya kazi hapo. Na wametoka sehemu za mbali.

Com. Lenaola: Tumeelewa hio.

Leah Abenyo: *na eponeta ngitunga ngulu ka ama. Sasa tokona kama nege eya ngabarafia neke na eponito ka ama*

Translator: Kwa upande wa bidhaa, tunataka Serikali isimamie bei ya bidhaa.

Leah Abenyo: alotoma ebei a akimuj. Alalar ebei a kimuj kisaki totuboi ebei a kimuj

Translator: Tunataka Serikali isimamie kila kitu. Kwa mfano zamani bei ya mabati ilikuwa chini, na kila kitu ilikuwa chini. Kwa hivyo tunataka Serikali iendelee kusimamia bei ya bidhaa.

Leah Abenyo: ata ngabawoi totuboi ibore daang ebei. Nakang nguna

Translator: Ni hayo tu.

Leah Abenyo: asaki akiyatakinii a lowahi alo ngaberu ka ngikiliok tangae iyanete ngiche tunga ebalasi kane aberu napeniusitae na tourito ka ekile ngide epederio kikotarai aberu ngina ka ngide toloto na nirumi aberu ngina emal a ekile ka ngolo. Aberu ngina na erotikinio ka ngide ngulle tarai kolong ekile ngolo auri ngide ngulu aluwahi eaari aberu ngina ngide ngulu. Si eliworosi ngide ngule ngimokorai (Clapping)

Translator: Tunataka wanawake wawe na haki sawa kwa mfano kama mwanaume ana wanawake wawili, hawa wote wawili, wawe na haki juu ya mali ya mwanaume huyo. Isiwe kuwa ati mmoja ameolewa rasmi, kwa hivyo huyo ndio ananafasi ya mali, katika nyumba hio. Wote wawe na nafasi sawa ya kugawa mali. Ikiwe lolote limetokea katika nyumba hio.

Leah Abenyo: *mere kimiekainai ikangari nahara kongina. Nakang daang nguna*

Translator: Isiwe kuwa ati yule hajaolewa rasmi ndio hana nafasi.

Com. Lenaola: Asante Leah. Daniel Amojo'ng. Repeat your name again halafu endelea.

Daniel Amojo'ng: Majina yangu ni Daniel Amojo'ng. Ningependa kutoa pia maoni machache hapa ingawa mengi yamenenwa.

Ya kwanza kulingana na vile tulivyo na sehemu tatu ya wakilishe Bungeni kama vile ambvyo imependekezwa, na mimi pia ningependa kusema kwamba Electoral Commission wametumia idadi ya watu, pengine ka kugawa na sehemu yetu hii ya Turkana ni sehemu kubwa. Kwa hivyo wakitumia idadi ya watu, tutakuwa, ama tutabaki nyuma. Lakini wakitumia factor ya ukubwa hata sisi tutakuwa na hio sehemu tisa, au zaidi, au nne ama tano na kwendelea. Wakitumia yaani upana. Lakini wakitumia idadi ya watu kama vile ilivyo sasa, tutakuwa disadvantaged.

Inginge pia ingekuwa wakati ya ambapo, Mbunge anaondoka ofisini, au Diwani anaondoka ofisini, lazima kuwe na handing and taking over exercises properly. Yaani huyu anaondoka ofisini na huyu mwengine anachukuwa ofisi mpya pamoja na mambo yote yalio katika hio ofisi.

Kama vile ambavyo wengi wamenena juu ya land, ingekua ni bora pia, yaani ardhi itawaliwe au isimamiwe na wenyeji na hasa iwe ni council ya elders.

Kuna sehemu zingine pia huwa ina, wakati mwengine Serikali ama Serikali yetu inaweza kupata rasili mali inaweza kupata madini, inaweza kupata dhahabu, na watu walikua wamefanya nini? Wamejenga hapo. Kama hio madini, au dhahabu imepatikana mahali pale, wale watu wakihamishwa kutoka hapo na wazo walipwe vizuri saana. Hawa watu ambao wamehamishwa kutoka hio sehemu, walipwe ma millioni ya pesa ndipo waondoke watafute pahali pengine na Serikali nayo ikichukuwa hio sehemu, kufanya kazi yake.

Pia katika ofisi ya ma Chief, kuelekea mpaka huko chini machinani, tunawatu tunaita wazee. Wazee, wanafanya kazi kutoka huko machinani mpaka kwa ofisi ya Chief, na hawa watu, huwa hawana hata mshahara. Lakini tungependa hii Katiba sasa ipea hawa wazee heshimas. Ipea hawa wazee heshima ya kupeyana kitu kidogo kama hata mshahara ama allowance kwa ajiri ya hawa wazee. Hiyo, Katiba mpya ifanye hivyo. Halafu hawa wazee watakapo fanya kazi, suluisha mambo ya wananchi kutoka kule machinani mpaka hapo juu watakuwa wako na nini? Na miyo ya kufanya kazi kwa bidii, na kwa wakati wote. Hata bila kufanya nini? Hata bila kuchelewa kuja kusaidia wananchi wakati ambapo wanataka huduma yao.

Halafu pia, lugha yetu ya kiasili kama kwa mfano, Kiturkana, Kinandi, Katiba ipewane heshima kwa lugha yetu ya kiasili. Kwa mfano lugha yetu hii ya Kiturkana ifunzwe pia katika mashule yetu. Katika darasa la kwanza au katika hata shule ya malenzi

Kiturkana ifunzwe na hii Katiba ilinde lugha hio ya kiasili ili tufanye nini? Isipotee mbali na lugha ingine ambae uwa inafanya nini? Uwa inangia wakati watu wamerevuka na wamesoma zaidi. Kwa hivyo lugha yetu ya Kiturkana au ingine yoyote ilindwe na Katiba.

Com. Lenaola: Endeal kumaliza tafadhali.

Daniel Amajo'ng: Pia tungependa kulingana na mambo ya mishahara kwa wafanyi kazi kwa sababu inatengenezwa na Bunge, kuwe na Kamati ambae inafanya nini? Inaamua mishahara ya wafanyi kazi wote kwa wakati mmoja. Mishahara ya wafanyi kazi iamuliwe kwa wakati mmoja kwa wafanyi kazi wote. Sio wengine kwa wakati ingine halafu wengine wanabaki wakiongojea wakati wao sijui itakuwa wakati gani. Wanaendelea kuwa na moyo mbaya na maneno mengine mengi. Kwa hivyo mishahara iongezwe na ma Kamati halafu na iwe ni wakati mmoja tu mishahara kwa wafanyi kazi wote wanafurahi, na wanafurahi kutoka huku juu mbapa huku chini.

Halafu pia kwa Wabunge wawe na ma ofisi katika hata sehemu za uwakilishi Bungeni kwa ajili ya kuhudumia, ningependekeza hivyo, ya kuhudumia wananchi. Asante sana.

Com. Lenaola: Ngoja, kuna swalii.

Com. Yano. Bw. Chief, hasa tukohapa venya wenging watu wetu wenging walikuwa wanasema ati wanetaka Chief kuwa elected. Uko na maoni kuhusu hayo. Na pia, ndio wakati huu tunajua Chief's Act imeondolewa, how do you do your work? Na umeridhika na venye unaendesha kazi saa hizi bila hio Chief's Act?

Daniel Amojo'ng: Asante saana. Hata kwa sababu ya wakati, umoja wapo ya point yangu pia ilikua ni kwamba hata sasa mimi natoa maoni, sisi pia tuchaguliwe.

Com. Lenaola: Kwa miaka mingapi?

Daniel Amojo'ng: Mimi singependa kusema tuchaguliwe kwa miaka mitano. Tuchaguliwe na tukaye kwa huu muuda wa miaka mpaka hamsini na tano.

Com. Lenaola: Hayo ni maoni yake. Sawa.

Com. Yano: Endelea.

Daniel Amojo'ng: Halafu pia kulingana na hilo swalii lingine, kweli kazi yetu sasa, kazi yetu kufika mahali pengine kwa sababu

ya hio Act kuondolewa, hata kazi yetu pia imekuwa rahisi. Kazi yetu pia imekuwa rahisi kufika mahali pengine. Kwa sababu tulikuwa na kazi mingi ya kufunga mabusu, katika ara zetu ama katika ma ofisi yetu. Kwa vile sasa hio Act imeondolewa imekua sasa nikatika idara ya Internal Security. Hata sisi kazi yetu imekua rahisi. Asante sana.

Com. Lenaola: Asante kwa maoni yako. Asante Chief kwa maoni yako. Tunashukuru. Councillor Joseph Okee. Joseph Okee. Mimi ndio najua Mimi ndio naendeleza mkutano. Si wewe. Mkutano ni wangu. Endelea.

Joseph K. Okee: Asante. Kwa majina ni Joseph A. Okee. Yangu ni machache. Ya kwanza ni kuhusu wanyama. Kidogo ningeongea na lugha ambae Waturkana wanasi kia halafu huyu atafsiri kwa Kiswahili.

Joseph Okee: *ewa a ngiteng. Eya ngitieng lu enyaritae ngaigirae ka ngikwei enyemete ngibaren a ngiturkana tabala nangolenyang niar*

Translator: Maoni yake ya kwanza ni juu ya wanyama ambao wanakula wanyama wengine kama mbuzi, wanakula mali ya Waturkana. Tunataka Serikali i compensate wale watu ambao wanyama wao wameliwa.

Joseph Okee: Maoni ni kwamba, mnyama yoyote ambae inahu kukula mnyama mwengine ambao inakuliwa na binaadam, instahili Serikali alipe. Hio ndio maoni yangu kuhusu wanyama. Na ngarei

Com. Lenaola: Haya Councillor sasa endelea tu na Kiswahili (the rest is inaudible)

Joseph Okee: Hapana. Iko wazee hapa wanangoja kusikia ile kitu ---

Com. Lenaola & Com. Yano: Unazungumuza na sisi, si na wazee. Leo si mkutano wako wa ki Councillor.

Joseph Okee: Lakini si ni mzuri wasikie -----

Com. Lenaola: Unazungumuza na sisi. Toa maoni yako kwetu si kwa wazee wako. Mukutano wako wa siasa ongea na wao.

Joseph Okee: Basi, ya pili: Kuhusu maneno ya uchaguzi. Ma Councillors wachaguliwe kwa laini (mlolongo),

Com. Lenaola: Endelea.

Joseph Okee: na awe mtu hajasoma.

Com. Lenaola: Endelea Councillor, endelea.

Joseph Okee: Ya tatu: Ma chief pia wawe wakichaguliwa na ma laini. Na awe mtu hajasoma. Ati akiwa amesoma ni sawa. Na ikiwa hajasoma ni sawa. Bora anatosha kuongoza. Kwa sababu tunawenza kuacha mtu ambae hajasoma na kumbe anastahili kuongoza na tunatarajia kalamu. Kalamu hii ni uongo hii mambo ya kalamu. Unaandika tu yule mtu hata ajui kitu. Kwa hivyo wacheni hata tutumie akili. Kwa sababu mtu ana uongozi ambae amezaliwa naye. Sio tu kusema ati amesoma na wale hawajasoma watapata mavuno namna gani kwa hii Serikali? Ni kama hii Serikali itatupa hawa. Kwa hivyo hawa pia wakumbukwe. Sio wote ndio wamesoma. Na si wote wakienda shule ndio wako na akili. Wengine wanaenda shule lakini hawana akili.

Jambo langu la nne ni mambo ya Central Highland: Hii mlima tupewe sisi Waturkana kama wenyewe. Sio sisi tusimamiwe na Samburu District na mlima ni yetu. Mavuno ya hio mlima tupewe kama wenyeji Waturkana. Asante.

Com. Lenaola: Asante Councillor kwa maoni yako. John Eroo. John Eroo.

John Eroo: John Eroo.

Com. Lenaola: Endelea.

John Eroo: alosi ayong a kiroit apei ana kinyaraunitere sua nakwap na kingeduni ngakiro a ngde alukosi atamari ibore kimidi sua ngini anakwapin ibore arai ashamba kosi ngina. Ikonikoktu ni pese ikoni akal na kilepuniut sua kila akwar

Translator: Angependa kuongea juu ya mahari. Anachukiza mambo ya mahari kuwa mtoto wakike katika jamii Waturkana ni kama shamba kwa wazazi waka. Kwa hivyo mahari iendelee. Watu wanaohusika watoe mahari.

John Eroo: *yaani na ebunitor ekile ngolo atamar asaki ngide kang, kwai elemunit ngesi lu anakatokeng kainaki ayong arai etal ngolo ekimila kosi ekile loebuni tourik ikoku kang ani loengeri attachuna ayong ngitunga kang etan anawi kang*

Translator: Inaenda pia sambamba na juu ya watoto. Watoto watakuwa wake. Yeye attachukua watoto bunde tu msichana anapo wacha mvulana wake. Yeye anaamuwa kuchukua msichana pamoja na watoto.

John Eroo: akiroit alosio ngina mam nabo ache

Translator: Ni hayo tu.

Com. Lenaola: Ngoja, ngoja.

Com. Yano: Mzee John, niko na maswali mimili. Ya kwanza ni kuhusu kama hio kofia umevaa. Hio ni maneno ya culture, si ndivyo? Maneno ya utamaduni wako. Na haujaongea maneno ya kitamaduni na umevaa kofia ya utamaduni. Una maoni kuhusu hao. Halafu, kuna pia, pengine huyu msichana mwenye unaita ‘shamba’ akiolewe na mtu masikini ama aolewe na watu wenya hawajui maneno ya kulipa mahari, kama nikikupatia e.g. ni kama Marakwet, ukiowa mwanamuke pengine kazi ni kupeleka pombe kwa wazee wakunywe wafurahi hakuna mahari mengine. Uko na maoni kuhusu hayo? Un gesema nini juu ya hio?

Translator: ekasukout eya ngakingiseta ngarei kingisitai iyong. Atamar ichamunit iyong atamar ibore ni inapit iyong aorich ka luche, ejok kori erono. Akiroit na nangarei alotoma nginapen a ngiturkana ingolikinit iyong ejok kori erono. Ibu takae iyong kiana kidiama ikoku atamar ilemari iyong ngibaren kori ngide na ache pak eyei ekibotonit lu a ngitela a luche ingolokinit iyong kwai, nyo tokona ilimuni iyong kidiama ikoku ngini kotere ngiche tela ku ikote ngimarakwet eyanario epurot bon

John Eroo: *kotere na iusia ngesi ikang koku agile ngesi amotoga alosio I awi ni eyei toma nawi bu ekile touriki ikoni robo ngini ikoni akal na alepi ayong jik*

Translator: Ametafautisha kuwa mtu akija kuowa msichana wake, mtajiri anaowa na anachukuwa msichana wake anaenda naye. Lakini yule pengine si mtajiri na anampatia mtoto huyo mimba na baado anakaa kwake, ye ye ataendelea kuchunga na kulisha hawa watu wawili na sasa hata consider kama hawa watoto ni wa yule mwanaume ambae ametoa --- Ni hayo tu.

Com. Lenaola: Joseph Lobolia. Lobolia.

Joseph Lobolia: Kwa majina naitua Pastor Joseph Lobolia na hudumu na Kanisa ya Redeemed. Naongea juu ya Banks zetu ile iko katika Kenya. Hata nchi zetu za nje. Ningependekesa bank iweze kuwa na kitabu, sio tu sasa kama Wilaya Turkana au nchi zingine, unakuta Bank, wewe umeweka pesa yako na umepata shida kule sehemu kama ya Kitale au na nchi ingine na wewe kweli uko na pesa kwa Bank, nilikuwa napendelea Bank iweze kuwa tu mahali popote Kenya unaweza kutoa pesa yako au hata kama ni America unaweza kupata pesa zako kama uko na kitabu cha bank.

Interjection ---(In audible)

Joseph Lobolia: Baado. Ya pili: Mambo ya kupata Passports. Nilikuwa napendelea kwa maoni yangu, Passport umepata Passport sio unaenda tu unaweka mtu mwingine akuwekee guarantee ati ndio pengine uende nchi za ng’ambo. Unaenda kwa mtu mwingine ndio anakuwekea guarantee. Nilikuwa napendelea iwe ni kama Chief anakuwekea au wazee wa ile area ndio

wanakuwekea, wanapitisha huyu ni mtu wa fulani.sio unaenda process mingi. Unaenda kwa Chief, ati baado tena utoke kwa Chief, unarudi tena mpaka kwa garantor mwingine anakusimamia naonelea hiyo jambo itupuliwe mbali.

Nitaongea mambo ya tatu: Nafikiri hata wengine wameongea juu ya Councillor. Napendelea Councillor awe ni mtu wa hio area. Wazee wa hio mtuu au wa hio Tarafa wajue huyo ni mtu wa sehemu, mtoto wa jamii fulani. Isiwe tu mtu kutoka sehemu ya Lokichogio ndio anakuja anasema ati anakuwa Councillor hapa. Na sehemu hizo zingine napendelea mtu mwenyeji wa hapo, huo area aweze kuwa anachaguliwa na wananchi. Na wazee wajue.

Mambo ya nne: Plot: Plots ninaonelea iwe ni wazee wale wa zamani wale wanajua huyu ni mtoto wa fulani, baba yake ni fulani ndio waweze kupewa plot au mchango wa hio area. Unaweza kuta saa hii mtu kutoka Kisumu au kutoka nchi zingine. Anakuja anapata plot hapa. Na mimi ni mtu wa hapa. Mtoto wa hapa ninakosa kupata haki yangu. Napendekeza kwamba plot iwe ni ya mtoto ule amezaliwa katika area.

Com. Lenaola: Endelea.

Joseph Lobolia: Upande wa kuabudu ama upande wa makanisa. Nashangaa na ningependekeza ya kwamba kama kweli tumepewa haki wakuabudu katika makanisa, ni kwa nini tunaenda tena mpaka kwa DO, ati ndio unachukua baruwa ya kufanya Injili kama kweli tumepatiwa haki? Tunataka tu kama tumepatiwa haki, tuhubiri Injili bure kwa sababu hakuna kitu tunapata. Tunatangaza tu msimamo wa Mungu, vile Mungu ameumba nchi. Kwa hivyo nilikua napendekeza iwe njia kwamba ya kuenda mpaka kwa DO, na wapi processes mingi, iondoewe. Kama ni Injili tunafanya tu bila kwenda kwa processes mingi. So hayo ndio yangu.

Com. Lenaola: Asante Pastor. Hebu jibu swali mmoja. Nimesikia mahali pengi kwamba uhuru wa kuabudu ikatwe kidogo maana kuna makanisa nyingi ambazo hata kuabudu kwao kuna wasi wasi. Unasema nini kuhusu jambo hilo?

Joseph Lobolia: Nawenza ----- uso wangu ya kwamba kama kweli Chief wa hiyo area anajua hii Kanisa aendi katika njia ya kuabudu au aiendi kuharibu kimila fulani katika hio area, kweli hawa hawa viongozi wa hio area, wana right ya kuondoa hiyo dhehebu mahali pale.

Com. Lenaola: Asante sana Pastor.Logen Ekaal.

Logen Ekaal: Kwa jina naitua Logen Ekaal. Maoni yangu ya kwanza nafikiria hii Katiba inatengenzwe mpya sio ya zamani, na maoni yangu ya kwanza inasema hivi. Nafikiria sheria ile ya zamani imetunyanyasha. Sheria ya zamani imetunyanyasha sisi saana. Ile kitu ninataka kuongea ni juu ya County Council. Saa hii mimi ni Mkenya na sii hii ninataka kuchukua plot mahali. Hapa Turkana, unaambiwa lipa kwanzia 1992 mpaka 2002. Mimi sheria ya zamani hio ni mbaya saana, wale walitengeza.

Com. Lenaona: Pendekteza.

Logen Ekaal: Sasa ningetaka tu, mtu akitaka kuchukua plot, saa hiyo anaambiwa ni pesa fulani kwanzia siku hiyo. Mimi nilikuwa nataka namna hiyo.

Halafu ya pili: Mambo ya stima. Mimi naona sheria ya stima imependelea pande ya down, kuanzia West Pokot irudi huko. Ingetakana tu stima igawiwe mahali popote Kenya. Ningependezea hivo.

Halafu meno yangu ya tatu kuhusu sisi Waturkana, kimila ya Turkana. Kuhusu mambo ya mahari. Mimi naona sisi wavijana Waturkana tunanyanyashwa saana kwa sababu vile tuko hapa tuko sawa, msichana na mwanaume, tuko sawa. Kwa sababu tukifika kwetu hapa tunaona msichana ndio iko equality ile equal right. Na sisi wanaume tunanyanyashwa kwa sababu tunasema hivyo kwa sababu ya mahari. Mimi nalipa mahari halafu mtoto anachukuliwa, mahari inachukuliwa mwanamuke anaenda na wewe unakaa kavu. Ningependezea hivi, kama ni mali wachukuwe, mimi nibakie na watoto. Hio ndio maoni yangu.

Com. Yano: Ni maoni yake mzee. Hayo ni maoni yake.

Com. Lenaola: Sawa, sawa. Asante. Nafikiri umeweka mzuri. Mwalimu Turfosa Atieno. Turfosa Atieno.

Turfosa Atieno: Asante. Jina yangu ni Turfosa Atieno. Mimi naongea kama Mkenya. Kwanza ninataka kuongea habari ya wanawake. Mimi ni mwanamuke na bwanaangu akikufa na saa ingine ako na mali, alipokufa hivi, mandugu wa bwana wanana mali yote wanachukuwa, mimi nabaki na watoto nikiangaika. Sasa Wakenya wewe kama Katiba kamba mali yote ya bwana ni ya bibi na watoto. (Laughter)

Com. Lenaola: Endelea.

Turfosa Atieno: Ya pili: Habari ya watoto wadogo kuanzia miaka mitatu mpaka miaka saba. Kitu inaitua Child Development: Serikali ya Kenya inajua Child Development ni nini. Na wenye hawawezi kuangalia mambo ya watoto wadogo kuanzia miaka mitatu mpaka saba kwa masomo yao na hapa ndio unatachia mtoto apate elimu yake ya kutosha na kesho awe mtu. Huku wanasema wamama wapange uzazi. Na njia ya watoto hawa, uzae watoto watatu na wasome vizuri, Serikali ya Kenya aitaki kujuwa. Sasa wanataka mtoto asome klas one ndio wakubali kupewa mtoto mwalimu ya kulipa pesa. Na hio ya Nursery Serikali aitaki. Na mtoto akifika mwaka saba hakuna kitu atapata because there is no foundation kwa huyu mtoto mdogo. Sasa wamama tunazidi kuzaa watoto wengi kwa ajili ya, tunazaa wengine wawe waizi, wengine wawe namna gani? Ni hivyo. Pendektezo yangu nilikua nataka hivi. Serikali iamuwe isaidia watoto wadogo kuanzia miaka mitatu mpaka saba.

Ya mwisho ni upande ma Chief: Ninataka, mimi ningependekeza kwamba Chiefs wachaguliwe na mlolongo nyuma yao kwa kuwa hawa ma Chiefs ya young turks wanaumiza sisi kwa manyumbani zetu. Saa ingine, kuna shida kwa nyumba ya mtu. Ukienda kwa police, unaambiwa enda kwa Chief yako. Chief naye ni kijana. Hata ukifika kwake, labda yeze pia jana alikuwa na shida na bibi yake. Hakuna kitu atakusaidia wewe nayo. Sasa tungependekeza kwamba, Chiefs wawe wazee wale wameshaona mzuri, wale wataleta uhusiano kati ya manyumba za wezao pia pamoja. Ni hayo tu.

Com. Lenaola: Miaka ngapi?

Turfosa Atieno: Miaka ya Chief iwe thirty-five and above.

Com. Lenaola: Sawa sawa. Asante mwalimu. Hakuna swali. Ukajiandikisa pale. Izaak Ewalan Izaak Ewalan. Halafu James Ekirun fuata yeye. Sema jina halafu endelea.

Izaack Ewalan: Basi kwa jina ni Izaack Ewalan. Mimi ningependa Oh, jina baado?

Com. Lenaola: Sema tu kwa sababu ya record.

Izaack Ewalan: Kwa majina naitwa Izaack Ewalan. Kwanza ningependa kuongea kuhusu Rais maana nilisikia ya kwamba mtu akitaja kuhusu Rais kwamba Rais akifanya makosa, anastakiwe. Lakini kwa mimi sijaona tangu nilipo kuzaliwa, sijaona watoto wakistaki baba yao. Hata ikiwa amefanya makosa sijaona watoto wapeleka baba yao, kupeleka kwa mti ya wazee kusema kwamba huyu baba wetu ni mchawi. Walikuwa wakio ogopa wakijua tu wale watastaki ni wale wengine wa jirani zake, wale wa nchi zingine. Walikuwa wanaogopa. Kwa sababu hata kwa kitabu cha Mungu, kiongozi inaogopua. Anawekwa heshima hakuna kusatakiwa. Mimi ninasema hapo Rais awezi kustakiwa akiwa amefanya makosa.

Cha pili nikitaaja kwa upande wa ma Chiefs ya kwamba, Chief mkubwa iweko na Chief yake mdogo mmoja isiwe tu wanaweka Chief mmoja karibu assistants nne, tatu, sita, kumi. Sasa kazi hio aitafanyika.

Sasa ninaongea kuhusu upande wa shule, elimu. Elimu ni vizuri Serikali atupatie sisi nafasi tu watoto wasome bure kutoka klas ya kwanza hadi klas ya nane. Lakini ikifika Form I na kuendelea hapo tumenyane na mambo ya shule kwa maana hapo ndio mambo iko.

Com. Lenaola: Endelea.

Izaack Ewalan: Basi kuhusu upande wa mahari ya kwetu, ya wazee ya kwetu. Kwetu kulikuwako na sheria. Lakini kuuliza

ya kwamba ninani anatakana kupewa asante? Ni yule ambao ameleta faida ama yule hakuleta faida? Kwa maana mimi mwanaume nimeleta faida, nililetea huyu mzee faida na hakuna asante. Ananiwacha mimi niende bure bila mtoto, bila nini. Sasa mali yote ni yake. Watoto ni yake. Mwanamuke ni yake. Na mimi nitakuwa wapi? Na mimi nitakuwa wapi? Na mimi nimetoa watoto. Nimetoa kila kitu. Na sasa watoto ambao sasa wako katika shule, ni wale watoto wetu ambae sisi tunazaa ambae sisi tunasomesha. Na hawa wenyewe hawashuguliki juu ya huyo mtoto.

Com. Yano: Pendekeza.

Izaack Ewalan: Kwa hivyo juu ya hiyo tunahitaji kabisa Serikali ione mizao yetu na huyo msichana. Hawa wazazi wapate mahari yao na mimi nipate watoto yangu.

Sasa naongea kuhusu ya, nasikia mama mmoja akiongea kwamba wanawake wanatakikana kuwa sawa na wanaume tena nasikia kwamba anasema kwamba mwanaume wakipigana -----

Interjection Com. Yano: (in audible)

Izaack Ewalan: Ngoja tu, maoni, hiyo hapo, sehemu hio, mwanaume wakipigana na mke wake, ni sawa. Hiyo ni mambo yao. Hakuna sheria ya kustakiana. Isiopo kuwa tu yule ambao anaweza kuchezea mwanamuke kama mabusu. Huyo anapasa kustakiwa. Kwa hivyo ndio maoni yangu ambao ningeongea. Asanteni.

Com. Lenaola: Asante Bw. Ewalan. James Ekiron. James Ekiron. Simon Konyen. Simon Konyen. Paul Kurian. Paulo Kuria. Moses Baruwa. Moses Baruwa.

Moses Baruwa: Asante sana Commissioners. Na katika hii Katiba ambao mumekuja kuongea juu yake.

Com. Lenaola: Sema jina halafu endelea.

Moses Baruwa: Kwa majina ni Moses Baruwa. Nitaenda kuongea juu ya Elimu. Na katika hii elimu yetu, kuna mahali kama Turkana kwa mfano, imekuwa chini saana katika hali ya elimu.

Com. Lenaola: Pendekeza.

Moses Baruwa: Pendekezo yangu ni kamba elimu, ningependa mtoto asoma kuanzia darasa la kwanza mpaka darasa la nne, yaani Form IV bila malipo yoyote. Na labda akiendelea kuitimu elimu ya kwenda University, ndio iwe na malipo fulani katika University.

Juu ya Hospitali: Ikiwa tuko katika Katiba mpya, na tunataka kufuta Katiba ya zamani, ningependa Serikali ituletee hospitali ya Serikali yenyewe ambao hatuwezi kulipa chochote. Sisi hapa tunaumia kwa saa hizi. Tunalipa ma hospitali ya wenyewe. Kwa hivyo ningependa Serikali ituletee hospitali ambao ni yake, na ni ya wananchi.

Juu ya Power: Mimi ningependekeza Serikali ya Kenya, itukumbuke sisi Waturkana na power. Kwa sababu tuko na power lakini inaenda mahali pengine ambao hatuja jua ni kwa nini. Kwa hivyo power ikuje kwetu ili tupate kusaidiwa au kufadiki katika ile moto.

Juu ya maji: Kuna areas zingine ambayo hatuna maji hapa kwetu na ningependa Katiba iangalie mambo ya maji. Kama Serikali iko na pesa fulani yakusaidia miradi ya maji, kwa mji fulani au kwa Wilaya fulani, sisi pia lazima tukumbukwe saana kwa hali ya maji kwa sababu kuna wengine saa hii wanamumia kiu mahali fulani fulani. Kwa hivyo sisi tunahitaji maji.

Bara bara: Sisi hapa Turkana tuko nyuma saana na maendeleo nyangi saana. Na ningependa kusema Katiba yetu hii mpya ambae tunabadilisha, ikianza kufanya kazi, sisi pia tukumbukwe na kitu kama bara bara. Serikali ituwekee bara bara kila sehemu ambao wananchi wako.

Juu ya Vyama ambazo zina tawala. Kwa mapendekezo zangu ningependa utawala wetu ya vyama hizi mengi. Mimi ningependa tu, tuwe na vyama mbili katika utawala wetu. Kwa sababu hizi mengi, mimi naona hata hazisaidii hata katika maendeleo.

Neno lingine ni kwamba, kuna watu wengi au kuna viongozi ambao wanafanya kazi mingi na wengine wamekosa kazi. Katika Katiba ya Kenya, ningependa kila mtu mmoja awe na kazi moja. Halafu wengine, wapate nafasi za kupata hizo kazi huyo mtu anafanya hizo nyingi.

Neno ingine ni kwamba mafuta. Nilisikia kwamba hapa Kenya sehemu kama Turkana hapa kuna mafuta. Na hii mafuta nimeshidwa hajjatekelezwa ama aija chimbwa. Na ilisemekana kuna mafuta hapa Turkana. Na hii mafuta pengine ikipatikana hapa Turkana, labda umasikini yetu wengine itapunguka. Lakini tumeshidwa, ilisemekana mafuta itachimwa na itaenda kufanyiwa mahali fulani. Lakini hio sasa ninaona aisaidii. Lakini kama ni Katiba mpya ambae tunafanya, mafuta ikiwezekana ipatikane hapa kwetu, ili tupate nafasi ya kazi.

Com. Lenaola: Jambo la mwisho. Last two points.

Izaack Ewalan: Neno la mwisho World Vision. Kwanza tukikuja kwa mfano hapa Turkana kwetu, itusaidia saana kwa hali ya juu. Maana watoto wako katika sponsor na sponsor uko anasema mtoto huyo afaidike na mzazi waka. Lakini, katika huo

usaizidi haisaidiki vizuri. Mtoto tu iko kwa sponsor lakini mzazi afaidiki na chochote. Hali kadhalika mzani ana ambiwa kwamba afanye cost sharing. Sasa mpaka unaangaika utafanya gani na gani? Ni hayo tu. Asante.

Com. Lenaola: Asante. Samuel Emankor. Daniel Achia. Hata umefika tu saa hii? Say your name and proceed.

Daniel Achia: Kwa majina naitua Daniel Achia. Si ongei mengi. Yale yenza nilikua nae, watu wameguza, guzia kwa kuwa kuna upande ambae inafaa niguze kidogo amba Serikali inafaa kabisa iangalie. Ni hasa hapa kwetu Wilaya ya Turkana, kuna shida minge saana. Kama wakati mvua inaweza kuwa imenyesha kama this time nyingi, unapata ma bara bara ni shida. Magari kupena chakula kwa ma Divisions zingine, ama Locations. Watu kuhama ni mifugo ni shida. Hayo yote inaelekea upande wa matibabu.

Com. lenaola: Toa pendekezo.

Daniel Achia: Pendekezo ni kwamba inafaa Serikali wakati mvua inapo anza, ituwekee kitu inaitwa mobile campaign ama Chief yakutembea na madawa ya mifugo na ya binaadam.

Halafu ya mwisho, nikuguzia upande wa ma Councillor. Tukisema ya kuwa ati iwe tu mtu ya Form IV. Mimi naona watu wameguzia maneno ya Form IV pekee yake, target yao ni Form IV, Form IV. So itaonekana ya kuwa haja gani tuende kuanzia masomo Primary. Councillor awe akisimama akiwa kutoka darasa la saba, nane hadi level inayo takikana kwa maana hawa watu pia ni ya muhimu, watu wa muhimu. Yeah.

Com. Lenaola: Asante mwalimu. Emana Lusikemoi. Emana Lusikemoi. Sema jina.

Emana Lusikemoi: Emana Lusikemoi.

Com. Lenaola: Haya sawa. Endelea tu.

Emana Lusikemoi: asaki eruoriki kidiama epak lokoi logo. Kidemasi sua ngitunga luche lu a Ethiopia ka ngiupe akop kosi. Kisaki nangolenyang kingoliki ngakiro nuku

Translator: Anaongea juu ya mipaka. Mipaka yetu ya Waturkana, ya Waturkana pamoja na jirani wetu wengine kama ya Pokot, Ethiopia, wametunyanyanya. Kwa nini Serikali imeachilia nafasi kwa hawa watu kunyanganya mipaka yetu.

Emana Lusikemoi: ngakiro a ngide. Eyakari ekile likauren ngide aloalom kidiama ngide keng tani bo kibootonit ngesi kotere ngesi idounit kechi

Translator: Anaongea juu ya mahari. Anaseka kuwa yule mtu ambae anaowa msichana wake, ye ye pia ananafasi ya kupata haki kwa yule mtoto ambae amemzaa. Ana nafasi. Kwa hivyo ye ye pia hata tupwa. Kwa hivyo hata kama ye ye ni masikini na wale watoto wamerudi kwaka, amewalisha na ye ye, yule baba ya hawa watoto baado ako na nafasi, ako na haki juu ya hawa watoto.

Emana Lusikemoi: erungo ngide ngulu arai ngika ekile

Translator: Juu ya mahari, baado tu watoto watakuwa ni ya wanaume.

Emana Lusikemoi: kisaki nangolenyang kingaraki kotere akamu akop nakosi angiturkana

Translator: Tunatake Serikali itusaidie kwa njia ya maji kwa sababu Wilaya yetu ya Turkana iko kavu. Kwa hivyo tunataka Serikali iweze kutuchimbia maji kwa wengi.

Emana Lusikemoi: na esal

Com. Lenaola: Jambo la mwisho.

Translator: ebeyo tolim akiroit na eal

Emana Lusikemoi: kisaki nanolenyang kiyataki ngakopin a nimjumbe ka ngikansolai alo turkan

Translator: Tunataka Serikali iongoze habari ya ma Wards ama Constituencies katika Wilaya yetu ya Turkana.

Com. Lenaola: John Lomodei - Chief. John Lomodei. John Lomodei.

John Lomodei: Kwa jina ni John Lomodei Ajie. Jambo la kwanza na nitajaribu kwenda haraka, haraka.

Com. Lenaola: Sema jina kwanza.

John Lomodei Ajie: John Lomodei Ajie. Jambo la kwanza ni juu ya Locational boundaries. Ningependekeza maana nimejaribu kuona upande wa Locations, wakati Chief anaandikwa, anaambiwa hapo ndio sehemu yako, Location ama Sub-Location lakini boundaries zinakuwa shida. Unagongana na Chief mwezanko mwenya munapakana naye. Kwa hivyo ningependekesa ile ofisi ambae inahusika na mapping, kama ni Survey, wa update mapping wa Locations ili administration isiwe

na shida ya mipaka.

Jambo lingine ni kuhusu border ya between Marsabit na Turkana kwa upande wa bahari ya Lake Turkana. Bahari tunasikia kwamba ni Lake Turkana kwa jina. Tunasikia watu wakisema hii ni bahari yetu. Lakini ukiangalia katika mpaka, unaona sehemu ya Turkana, yenye iko kwa Turkana ni kidogo saana, ni a quarter. Bahari yote iko Marsabi. Sasa tunaone sisi, ni kama sisi tunapigania hapo hii gulf tu inaitua Pagazone Gulf. Kwa hivyo mimi ningependekeza boundary ya Marsabit na Turkana kuititia kwa bahari iwe reviewed angalau kama ni kugawa kati kati, tugawe.

Jambo lingine ni kuhusu ofisi ya Ombudsman's office. Ningependekeza hio ofisi pia iweko katika, ikiwezekana kwa District level ili wananchi waweze kupeleka shida zao na waweze kuhudumiwa.

Mambo ya Districts: Hapo tangu uhuru, tangu kabla ya uhuru, tumekuwa na District moja. Na tumekuwa na kiwangu sub-district tangu kabla ya uhuru. Kwa hivyo ningependekeza Lokita'ng iwe promoted iwe District. Na pia sehemu zingine ambae inawezekana. Tuwe na District angalau tatu.

Jambo lingine pia ni mambo ya Constituencies: Ningependekeza kila Constituency iwe divided tupate angalau wajumbe sita ama zaidi. Tusiangalie saana mambo ya idadi ya watu, maana sehemu yetu hapa ni kubwa. Kwa hivyo kuhudumia hawa watu wanasema ni wachache baado ni shida. Kwa vile ni kubwa na Serikali ingependa huduma ifikie wananchi, basi Serikali isiangalie saana mambo ya idadi ya watu. Pia waangalie distances.

Jambo lingine ni kuhusu mambo ya heritage ama ile kuridhi. Mambo ya uridhi ningependa kuguzia kwa upande wa District yetu ya Waturkana. Kwa sehemu zingine sioni shida. Mtu akikufa, jamii yake wanaridhi mali. Lakini, hapa kuna shida kidogo. Ndio maana unaona watu wengi wanaongea mambo ya uridhi. Utapata kwamba katika desturi zetu, ama kimila yetu. Kimila yetu aitambui hii harusi ingine kama ya Kanisa, ama pengine wanaenda kwa Koti ama kwa DC. Lakini ile ya kienyeji ndio wanatambua. Na unaona inasumbua sisi kwa sababu watu wengi wako kwa ile ya kienyeji. Sisi tu wale tunaenda town ndio pengine tunaona ile ya Kanisa ni sawa. Tunaona ile ya DC pia ni sawa na namna hio. Sasa hapa ningependekeza iwe na Kamati ya wazee wenye wanahusika na hio kazi kwa ofisi ya Chief. Tukiwa na hio shida, wanakaa chini, waangalie ni nani anafaa kuridhi ile mali. Wasinyanyase upande mwengine, pande pengine wa msichana ama upande wa kijana. Wanajua, wazee wakikaa chini, watafanya vizuri bila kupendelea.

Com. Lenaola: Saa ni mbaya bwana.

John Lomodei: Umeniharakisha tena. Okey, wacha niende kwa ile muhimu, muhimu. Kwa mfano mambo ya irrigation. Unaona kama sehemu hapa ya Turkana ni kavu na kuna sehemu zingine inaweza kufanya vizuri kwa ukulima inakuwaga too much. Kwa hivyo sisi ningependekeza, Serikali iangalie sehemu ya nchi yenye inaweza kufanya vizuri katika irrigation. Ifanywe

hio irrigation ndio watu waweze kufaidika. Kwa mfano hapa Turkana kuna sehemu nyingi baadala ya kila siku kupewa chakula ambae ikikuja watu wanabaki tena wanarudi katika ile hali. Watafute njia yaku inua ama ku improve ile mahali ambae inaweza kulimwa na wafanye irrigation ndio watu wafaidike ndio itapunguza ile mambo ya umasikini.

Kwa hivyo mambo ya research naye ingepatia wazee. Kwa sababu hapa kuna ile kuhama, hama.

Mambo ya Title Deed pia ingekua kwa towns tu. Lakini uko nje ibaki vile livyo na wazee wawe wamechaguliwa katika Locations ya kuangalia mambo ya area yao. Kwa sababu wanyame wetu wana hama, hama. Wanaenda Loima. Wanaenda Lodwar. Wanakuja hapa Kalokol kama iko nyasi. Kwa hivyo ningependekeza ibaki vile ilivyo, lakini wazee wawekwe pia.

Na mambo ya corruption, mambo ya corruption watu wanaimba tutoe corruption. Lakini hawasemi tuifute kwa namna gani? Mimi ningependekeza kwa sababu ni wafanyakazi saana ndio wana husika na mambo ya corruption, ma ofisi kama pengine ya Chief, pengine Police, pengine wale ambao wana hudumia wananchi, ningependekeza hawa watu, Serikali iwe ikiwalipa mshahara nzuri ili mtu akipatikana anafanya corruption, basi afanyiwe adabu yenyenye inatosha. Kama ni kifutwa, afutwe. Kama ni kustakiwa yule mtu, astakiwe, kwa sababu amefanya makosa. Lakini sasa mtu ambae iko njaa na pengine amepata chakula na munamchukuwa yeze makosa, sasa pia hautakuwa umefanya vizuri. Ni vizuri umfanyie vizuri na akigeuka hio, basi itakuwa makosa ni kwake.

Ya mwisho, ningependa NGO's yenyenye inakuja kwa sehemu, maana pia hawa wanapata pesa kwa hio sehemu ambae wanaenda, wangkuwa na percentage fulani, yenyenye wanapeana kwa hio sehemu ambao wako kwa mradi ya sehemu hio. Na angalao wafanyie kwa njia moja ama ingine, kama kuna pengine, kuna mradi pengine hospitali, pengine kuna mradi wa shule, project fulani, pengine ya wamama. Yoyote pia chenye wananchi wa sehemu hio watasema, wasaidie. Ili pia waone umuhimu ya hio NGO kwa hio sehemu. Kwa hivyo kuna zingine ningesema lakini saa ndio inatupeleka vibaya

Com. Lenaola: Asante sana.

John Lomodei: Kama hii ya ma chief. Hawa ma Chiefs pia ningependekeza pia ma Chiefs wapewe ile proficiency test kama ile ya ma DO waweze kuendelea. Unaona sasa Chief anaandikwa ata kama ni form IV na anapewa na yule hajasoma Grade mmoja, Job Group Grade II wanaanza hio na wanakaa hapo tu kama hakuna yenyenye anaangalia aende, huyu mtu anabaki hapo tu, hakuna namna yakuendelea. Ingekuwa na mtihani ambae anafanya ili aweze kuendelea.

Com. Lenaola: Asante.

John Lomodei: Asante.

Com. Lenaola: Asante sana kwa maoni yako. Daudi Uhuru. Daudi Uhuru. Halafu Paulo Natoo yuko? Paulo. Na William Totoo.

Speaker: William Totoo ndio huyu.

Com. Lenaola: Okey, basi.

David Uhuru Ong'awa: Kwa jina mimi ni David Uhuru Ong'awa na nitaongea machache.

Com. Lenaola: Straight to the point.

David Uhuru Ong'awa: Sasa. Kwa jina, mimi ni David Uhuru Ong'awa na nitaongea machache.

Com. Lenaola: David Uhuru nani?

David Uhuru Ong'awa: Ong'awa. Kwanza nitaongea kwa marurupu ya wafanyi kazi ya Serikali. Allowance, kila mtu iko sawa. Na unaweza kwa upande wa allowance kwa wafanyi kazi wa uma, unakuta kitu kama hardship allowance, pesa ya matibabu, unakuta hio pesa kuna wengine wanapewa mingi kuliko wenzao, na ugonjwa ni ugonjwa. Vile Bw. Chief anaweza kuwa mgonjwa ndio huyu mzee pia anaweza kuwa mgonjwa. Hakuna wakati pengine utakuta surbordinate staff ni mgonjwa kuliko PS au

PS ni mgonjwa kuliko surbodinate staff.

Com. Yano: Pendekeza.

David Uhuru Ong'awa: Kwa hivyo mimi napendekeza hivi. Allowance kama ni elufu kumi au ni elufu moja au ni mia tano, iwe sawa kwa kila mtu.

Upande wa salary, wenzangu wengine wameongea, salary kwa wafanyi kazi wa Serikali ni kidogo. Hio ndio sababu unakuta watu kama Police na watu wengine wenzao wanasesma wanachukuwa rushwa kwa watu. Mshahara ya wafanyi kazi ya Serikali iwe reviewed, wapewe pesa ya maana.

Maneno ingine pia wenzangu walisha ongea na mimi pia naona ni kitu cha maana, ni Waalimu wa Nursery: Waalimu wa Nursery wanatakikana waajiriwe na Serikali kwa sababu wana himiza elimu na hakuna mtu ambae anaweza kusomesha mtoto bila foundation. Kwa hivyo, waalimu wa Nursery wanatakikana waajiriwe na Serikali na mimi kwa upande wangu natarajia pengine kama hii Tume, baada ya kumaliza kazi yake hii, tukianza Serikali mpya, hio mambo itekelezwe.

Inging ni kwa upande wa retirement. Retirement age iwe sixty years instead of fifty-five kwa sababu siku hizi, wale watu wa zamani walikuwa na andika umri yao ya uongo. Siku hizi watu wameenda shule. Mtu kama alizaliwa 1960, ni 1960, kama ni 1958 ni 1958. Kwa hivyo unakuta kama mtu anasfafu kama baado ni kijana kabisa. Kwa hivyo isongezwe iwe sitini instead of fifty-five.

Inging ni land inheritance. Nikiongea juu ya land, ardhi, unakuta mimi iko na Title Deed na mwezangu kuna mahali kwa shamba nimenunua, na unakuta mimi iko na Title Deed na huyo officer pia iko na Title Deed na ukiangalia sheria, taratibu vile imewekwa na watu wa ardhi, kuna form unajaza, agreement form, na hio form, Chief ana sign. Baada ya hio unaenda kwa Land Board, Land Board, Mwenye Kiti ni DO, na baada ya hio, ukisha pewa ukienda hio process yote na upewe Title Deed, hio the same, same piece of land umenunua unakuta mtu mwininge pia iko na the same, same Title Deed. So unashindwa hii kitu iko namna gani? Sasa ningependekeza hivi, sheria ambae sasa intaundwa kuhusu ardhi, iundwe bila loophole yoyote.

Inging ni Government Quarters. Wale wafanyikazi wa uma ambae wanakaa kwa semi-arid areas. Kuna wengine wako na family yao down country au mahali pengine na wamekuja hapa na pesa ya nyumba ile anapewa ya marurupu ni kidogo saa zingine. Sasa analipa nyumba huko family yake wako, na hapa pia anatakikana aliye nyumba. Sasa, kama kuna sehemu, sana sana sehemu ya hardship areas, kama nyumba ya Serikali iko hapo, wafanyi kazi wa Serikali ambao wanafanya kazi iko, wapewe nyumbe na wakae free.

Constituencies: Mimi kwa upande wangu ninaona Constituencies iwe created kulingana na population. Kwa sababu kuna, ukiangalia sasa mshahara ya Wabunge, Wabunge wanalipwa pesa nyingi, na ukiwa Constituencies zinaweza tu created bila kuangalia idadi ya watu, hio itafanya Serikali itapoteza pesa nyingi. So, iwe proposed, kama Constituency iwe created kama idadi ya watu huko ni elufu thelathini au ishirini na kitu. Iwe kitu kama hio.

Com. Lenaola: Recommend the administrative figures.

David Uhuru Onga'wa: Mimi kwangu ningependekeza elufu ishirini na nne.

Inging ni utumishi ya pesa ya Serikali AI holders. Ai holders lazima apewe nafasi mzuri ya kutumia pesa yao. Pesa iletwe kwa District Treasury lakini AI holder awe na Account yake ya kutumia hio pesa kulingana na vili inatakitaka. Unaweza pata pesa imekuja, na kila AI holder iko na pesa yake na pengine kuna gari ya Idara fulani imeharibika, unataka hio gari itengenezwe irudi njiani, kupata hizo pesa, unaambiwa pesa baado hakuna, pesa baado hakuna, pesa baado haijakuja, pesa baado hakuna. So iwe namna hii: Pesa itoke huko Headquarters, iije kwa District Treasury halafu AI holder yake awe na Account yake. Vouchers iende through the normal process, lakini ikifika wakati wa kutoa pesa, a sign hio voucher, aende achukuwe hio pesa mwenyewe.

Com. Lenaola: Last two points.

David Uhuru Onga’awa: Last two points: Civil Servants wawe ma welfare yao. Halafu askari ya Serikali wapewe equal priorities. Unaweza kuta pengine tuko na Forest Guards, C Scouts na tuko na Administration Police na Kenya Police na wengine. Kuna wengine wamepewa bunduki na kuna wengine hawana bunduki. Hio ndio sababu unakuta insecurity iko. Kama kwa upande wa hii bahari, na kwa upande wa sehemu zingine wa forest. Management ya hizo resources inakuwa ngumu kwa sababu wale amba wamepewa kazi ya kulinda hizo vitu, hawana firearms. Na wale amba wanaharibu hizo vitu wako na firearms saa zingine. So, askari iko na kazi yake na ma askari wengine pia wako na kazi yao. Sasa, mimi ningependekeza kila askari, mtu yoyote anaitua askari ambae ameajiriwa na Serikali apewe firearms (word not clear). Nafikiri ni hayo tu.

Com. Lenaola: Asante Bw. David. Paulo Atoo.

Paulo Atoo: *ekang kiro Paul Atoo*

Translator: Kwa majina ni Paulo Atoo.

Paulo Atoo: arai epastait

Translator: Pastor.

Paulo Atoo: *ibore ni ekingareni ngesi akiwanja ikeny na alokichogio*

Translator: Jambo la kwanza ni juu ya wanza wa ndege wa Lokichogio.

Paulo Atoo: *arai kolong lokichogio ewai a turkan*

Translator: Lokichogio ilikuwa ni sehemu mmoja ya Turkana.

Paulo Atoo: tani naponeta ngakampunio turukaut arai aka ngiturkana

Translator: Ma Kampuni ya Lokichogio yalipo ingia ikapata Lokichogio tu ikiwa ni ya Turkana.

Paulo Atoo: asaki ngaraopiae daang na etachi UN alokichogio toliwor ingarakinere ngiturkana mere tolema nangolenyang

Translator: Amependekeza kuwa pesa zote ambazo zinalipwa na ma Kampuni ya UN ambazo ziko Lokichogio zote ziwe pesa za kusaidia Waturkana wenyewe sio pesa zakugawa kwa nchi nzima.

Paulo Atoo: *kane na elosoto ngitunga a kichiem a lowahi alo ngikoro kiriemunosi ka ngimoi luche lukaarak. Kisaki nangolenyang yau arieng lowahi lokosi loko kiyoko ngikechemak*

Translator: Katika ziwa hili la Turkana, wavuvi wanapo enda kuvua samaki ule uvuo mwingine wa bahari, sehemu za Marsabit, mara nyingi uwa wanapata shida. Wana wawa na Boran, Rendile na wengine wengi, ma adui wengine wale wako uko. Kwa hivyo ye ye angependekeza kua Serikali itoe security, security wa wavuvi amba owanavua kwa bahari, ikiwa kwa Waturkana ama kwa wale wengine.

Paulo Atoo: echamakina ngikatukok ka ngasikaria kechi ingaranete ayauni ekisil nege

Translator: Anapendekeza pia Chiefs, ma askari wawe katika mstari wa mbele kulete amani katika nchi.

Paulo Atoo: ache pak irukauni emisikinit nangolenyang ngituga esaa loejiete kechi kimie taarasi kongina

Translator: Kwa wakati fulani utaona Police akiona watu wakipigana, na ye ye ajali mpaka wakati ule watu wanaumiya, wengine wana wawa, ndio atachukuwa hatua. Kwa hivyo ----

Paulo Atoo: toliwor ngikatukok ka ngasikaria kechi ingarenete

Translator: Kwa hivyo ma Police, ma Chiefs wawe katika mstari wa mbele kulete amani.

Paulo Atoo: mam sua ngiboro luikote lu angakopini anache. Kisaki sua kiyunun a tv ka ibore daang

Translator: Juu mambo ya communication hapa Turkana inakuwa ni duni saana. Iko katika hali ya chini. Kwa sababu ukienda sehemu zingine za down country utaona kitu kama T.V., utaona communication ni sawa. Lakini ukiangalia sehemu za Turkana, unaona mambo ya Communication iko chini saana.

Com. Lenaola: Pendekesa.

Translator: ebeyo iyong tolil ibore nisaki iyong tosubakinai

Paulo Atoo: asaki yaunai a booster napelem a TV

Translator: Angependa booster iletwe hapa ya T.V.

Com. Lenaola: Jambo ya mwisho.

Paulo Atoo: nyo bo ingolaritor nangolenyang lowahi epe i bon. Na engerio ekile eberu kititakinai. Nyope bo ititakinere ngide luepolote kimiekis ngiure kech kaneni?

Translator: Kuna shida. Mzee anauliza kwa nini Serikali inalegeza nguvu zake kwa upande mmoja. Unaona wakati mwanaume anawacha mwanamke, ana divorce mke wake, Serikali inachukuwa hatua ya kwenda kumstaki bwana. Lakini ukiona watoto, watoto wanapo kuwa wakubwa, wanamwacha mzazi ambae pengine ni baba yao. Kwa nini sasa Serikali, aichukuwi hatua kustaki wale watoto kwa ku neglect mzazi wao.

Paulo Atoo: *tolemarai arusi ni ifanyeneo aloofis a DC kidogo na ekanisa kana lo raya bon*

Translator: Harusi ya kwa DC ama ya Serikali itupuliwe mbali. Iwe tu ni ile mbili. Ya Kanisa na ya kitamaduni.

Com. Lenaola: William Totoo. Hebu karibia mwezangu. Straight to the point.

Translator: ekang kiro William Totoo ekasukout a kijji

William Totoo: Anaitua William Totoo. Mzee ya kijiji. Kiyaki kare atipei

Translator: Anaongea juu ya wafanyi kazi wa Serikali.

William Totoo: *ngitunga lukolong efanyete ekas a nangolenyang toloto retire. Elemanarete kechi ngirwa lukalaak eroko neanyuna ngaropiae kech*

Translator: Wafanyi kazi wa Serikali, mara nyingi mtu aki retire, ye ye uchukuwa muuda mrefu saana kupata pesa zake ya retirement.

William Totoo: echamakina nangolenyang na eyenia atamar aloto iche twan retire tosubaki ngaropiae a itwan ka ngini atipei

Translator: Angependekeza kuwa Serikali, inapo jua kuwa mtu ana retire, atengeneze benefits zake haraka na immediately aki retire anapewe na anaenda kuanzisha maisha yake tena.

William Totoo: eyaunit ngakiro nu daang ngesi ngakiro na akiit na esaketa ngitunga kitachakakini idio bore

Translator: Huu mzigo wote imetokana na ile chain of command ile iko kati kati. Baadala ya mtu kufanya kazi yake amalizie yule mtu, aende retire kwa njia nzuri, yeze tena anataka bribery, anataka kufanyiwa mambo mengi.

Com. Lenaola: Point ingine. Tumeelewa hio. Chukuwa ingine.

William Totoo: kisaki yarai astima lowahi lo alo turkan

Translator: Tunataka stima ile elekezwa kwa upande wa Turkana.

Com. Lenaola: Aseme jambo lingine tafadhali.

William Totoo: *toliwor emasom eka pas kuansia nursry tananga form four*

Translator: Elimu iwe ya bure kuanzia Nursery mpaka kidato cha nne.

William Totoo: tarama ngitunga ekura tolemut ngikatukok

Translator: Chiefs wachaguliwe kwa mlolongo. Hakuna kufanya interview.

Com. Lenaola: Asante Bw. Totoo. Neenda ujiandikishe. Sasa wewe, jambo mmoja, huko, wewe jambo mmoja huko, sawa, sawa. One point na unaenda.

Hassan Ibrahim: Mimi yangu ni mmoja tu. Jambo mimi nataka kuzumuza ni moja tu, juu ya kipande. Juu ya kipande, zamani birth certificate ya watoto kwenda Sheria House inasumbuwa sisi. Sasa kipande kwisha too much kuliko hio. Sasa mapendekezo yangu ni kama hapana lete hapa kipande, aandike karani kwa kila district, moja, moja au mbili, mbili yaku tetea district yake. Yangu ni hio. Basi.

Com. Lenaola: Jambo moja. Umeona vile amesema Ibrahim? Wewe pia ile inakuumma roho saana, toa hio halafu kwenda ujiandikishe. Sema jina.

Jacob Eroo: Jacob Eroo.

Com. Lenaola: Jacob?

Jacob Eroo: Eroo.

Com. Lenaola: Eroo. Haya endelea.

Jacob Eroo: Mimi mapendekezo yangu nilikua nikiiongea maneno ya Turkana customary law. Kitu nilikua ningesema kwa mapendekezo yangu, ni ile sheria ilioko wakati ile wa Turkana customary law, ibaki tu namna hio, kwa sababu kuwacha kimila yake ni mtumwa. Sisi si wazungu. Sisi tuko mapendekezo ya kupindwa tu Katiba ya sheria pekee yake, ile maneno ambae tunataka kwa Serikali. Hatuendi kwa maneno ya nyumbani kwa kusaliwa.

Ya pili, ninge ongea juu ya kuhusu ziwa la Lake Turkana. Ingekuwa kama kwa mapendekezo yangu kama ingewezekana, Serikali ingesaidia sisi kutowa hio Bahari upande wa Marigat na kama hawawezi tunafanya cost sharing kati ya Marsabit na Turkana District. Asante.

Com. Lenaola: Asante sana. Huyo ndio musemaji wa mwisho. Ningetaka kuwashukuru saana. Tangu asubuhi tumeketi na nyinyi, maoni mazuri ya kupendeza. Tumeshukuru. Na kabla hatuja maliza tungemwita Pastor, wacha tusema maombi ndio tupate kumaliza.

Rev. Thomas Ekai: Tunataka tuombe. Tomuduko elipa

Asante saana wananchi kwa kufika hapa watu wa Mungu. Nyinyi ni watu wa maana saana. Nyinyi ni watu wa ajabu kwa hivyo tunataka tuombe na tuamini.

Mungu Baba, Mungu Mwana, Roho mtakatifu, tunakushukuru kwa sababu ya ulinzi wako. Tulipo anza tulikuita na sasa tumefika kwenye ukingo wa siku wa leo, tunaomba maoni ambao tumetoa kwa ajili ya kusaidia kujenja nchi hii ambao umetupa tuishi, Mungu yawe ya faida mbele yetu na hata mbele ya Commissioners ambae watakutana wakiweka pamoja. Mungu utubariki tunapoenda, tunapo wachana utuongozze kila mmoja katika jina ya Yesu alie mwokozi wetu naomba, AMEN. (In Kiturkana)

The meeting ended at 4.25 p.m.

KALOKOL INDEX FOR KITURKANA DIALECT

TAPE	I	Side A at the beginning	- Hon. David Ethuro
TAPE	I	SIDE A	- Com. Lenaola in greetings
TAPE	I	SIDE B	- MZEE ESNYEN YOK
TAPE	II	SIDE A beginning	- JOSEPH EKAL
TAPE	II	SIDE B towards end	- MARGARET KIPCHUMBA
TAPE	II	SIDE B	- Mzee AIYANEI ESNYAN
TAPE	II	SIDE B	- EDWARD KAZO
TAPE	II	SIDE B	- JAMES LATOR
TAPE	II	SIDE B	- ANNA AKUOM
TAPE	II	SIDE B	- EKOEL LONGESAN
TAPE	III	SIDE A	- MUSA MWOWESE
TAPE	III	SIDE A	- PHILLIP LOKWEN
TAPE	III	SIDE B	- MARIKON AMADI
TAPE	IV	SIDE A	- JOSEPH OKEE

TAPE	IV	SIDE A	- JOHN EROO
TAPE	IV	SIDE B	- EMMAN LUSIKON
TAPE	IV	TOWARDS END	- WILLIAM TOTOO
TAPE	IV	'	- PAULO ATOO